Imetolewa tarehe: 19 Oktoba, 2010

MAELEZO YA UTANGULIZI YA KAIMU MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA), HIITI B. SILLO WAKATI WA SEMINA YA UHAMASISHAJI WADAU WA TFDA KUTOKA MOAT, TABOA NA WAHARIRI WATENDAJI WA VYOMBO VYA HABARI, KUHUSU UDHIBITI WA MATANGAZO YA BIDHAA UKUMBI WA MAMLAKA, TAREHE 19 OKTOBA, 2010

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa,
Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA),
Katibu Mtendaji wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari (MOAT),
Wahariri Watendaji wa Vyombo mbalimbali vya habari,
Sekretarieti na watumishi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa,
Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha rasmi kwenye semina hii muhimu ya wadau wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA).

Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru wageni wetu waalikwa kwa kuitikia mwito wetu kuja kuhudhuria semina hii na kukubali kuacha shughuli zenu muhimu. Hiki ni kielelezo kikubwa cha jinsi mlivyo tayari kushirikiana na Mamlaka hii katika kulinda afya ya jamii.

Ndugu washiriki, wa semina hii, Mamlaka ya Chakula na Dawa ni taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu Na. 4(1) cha Sheria Na. 1, ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Mwaka 2003 iliyoanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai 2003. TFDA ilianzishwa baada ya kuunganisha taasisi mbili tofauti yaani zilizokuwa Bodi ya Madawa na Tume ya Kudhibiti Vyakula ya Taifa (TUKUTA). Taasisi hizi mbili ziliundwa chini ya Sheria ya Dawa na Sumu Na. 9 ya mwaka 1978 na ile ya Kudhibiti Ubora wa Vyakula Na. 10 ya mwaka 1978 ambazo zilifutwa na Sheria Na. 1 ya mwaka 2003.

Ndugu washiriki,

TFDA imeanzishwa ili kuimarisha huduma za udhibiti wa ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba bidhaa zenye ubora unaokubalika ndizo zinazosambazwa na kutumika nchini.

Mamlaka ina wadau wengi ikiwa ni pamoja na;-

- **Ninyi wamiliki wa mabasi na vyombo vya habari**
- **Wahariri watendaji wa vyombo vya habari pamoja na waandishi**
- **Watengenezaji, waingizaji nchini, wasafirishaji nje ya nchi, wasambazaji na wauzaji wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba**
- **Wasimamizi wa sheria**
- **Wafanyakazi wa sekta ya afya na watafiti**
- **Idara za serikali na taasisi binafsi**
- **Mashirika ya Kimataifa**
- **Mashirika yasiyo ya kiserikali**
- **Walaji, watumiaji wa bidhaa na wananchi kwa ujumla**

Mpaka kufikia leo hii, TFDA ina umri wa takribani miaka 7 na miezi mitatu (3). Pamoja na umri huu, bado haijafahamika vizuri na pia majukumu yake pia bado hayajulikani kwa wadau walio wengi ikiwa ni pamoja na baadhi yenu na wananchi kwa ujumla wake. Ili kuhakikisha kuwa inajulikana, Mamlaka imekuwa ikikutana na wadau wake kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu kazi mbalimbali za Mamlaka na majukumu ya kila mdau katika kutekeleza Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003. Moja ya mikakati hiyo ni kwa kufanya semina mbalimbali za wadau ambapo mara kadhaa tumekwishakutana na Wahariri na Waandishi wa Habari.

Semina hii ya leo ni ya kipekee kwani pamoja na kuhusisha wahariri na watendaji kutoka vyombo mbalimbali vya habari, inajumuhisha pia washiriki ambao hatujawahi kukutana nao toka kuanzishwa kwa

Mamlaka mnamo tarehe 1 Julai, 2003, hususani Wamiliki wa vyombo vya Habari na Wamiliki wa Mabasi.
Hivyo, tunategemea itakuwa na manufaa makubwa kwa washiriki hao na wengine walioalikwa, lakini pia kwa Mamlaka kama mdhibiti wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Ndugu washiriki, semina hii inafanyika kwa siku moja na malengo yake kwa ujumla ni pamoja na:

- **Kuwafahamisha washiriki kuhusu mahitaji ya sheria juu ya udhibiti wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba na kuweka mikakati ya pamoja ya namna ya kuisimamia na kuitekeleza kwa hiari;**

- **Kuwafahamisha washiriki kuhusu majukumu na kazi za Mamlaka ya Chakula na Dawa;**

- **Kuwahamasisha washiriki kuhusu umuhimu wa udhibiti wa matangazo ya bidhaa katika mabasi, vituo vya mabasi na vyombo vya habari na uzoefu wa TFDA katika kusimamia hili;**

- **Kuwaeleza washiriki kuhusu wajibu wa wadau katika kusimamia Sheria Na. 1 ya mwaka 2003;**

- **Kukuza ushirikiano kati ya wadau na Mamlaka ili kuboresha udhibiti wa bidhaa nilizokwishazitaja.**

Ndugu washiriki,
Ni matarajio ya TFDA kuwa mwisho wa semina hii mtaielewa vyema Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Na. 1 ya 2003 na majukumu ya Mamlaka ili muweze kushirikiana nasi katika kuisimamia kwa lengo la kulinda afya ya wananchi wote kwa ujumla ikiwa ni pamoja na sisi wenyewe, ndugu zetu, jamaa na marafiki.

Aidha, ni matarajio yetu kwamba tutaainisha kwa pamoja maeneo ya ushirikiano katika kuielimisha jamii kupitia vyombo vyenu vya habari juu ya mambo mbalimbali yahusuyo udhibiti wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Hii inatokana na ukweli kwamba pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa kupewa dhamana ya usimamizi wa Sheria hii Na. 1 ya mwaka 2003, usimamizi wake hautakuwa na mafanikio kama hatutawashirikisha wadau mbalimbali hususani vyombo vya habari na wamiliki wa vyombo vya usafiri.

Baada ya kusema hayo machache, napenda tena niwashukuru kwa kufika kwenu na ninawatakia ushiriki mwema katika semina hii. Napenda kutamka kwamba semina hii imefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza